# HALMASHAURI YA MJI MAFINGA

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MJI MAFINGA

Unapojibu tafadhali taja:

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

## 13/06/2022

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Mafinga anapenda kuwatangazia wananchi wote wenye nia ya kufanya kazi ya **Ajira ya Muda (Vibarua)** kwa nafasi zifuatazo:-

1. **WAKUSANYA MAPATO - Nafasi 33**

**SIFA ZA MWOMBAJI**

1. Awe ni Mtanzania na mkazi wa Mafinga.
2. Awe na umri usio chini ya miaka **18** na usio zaidi ya miaka **45**.
3. Mwombaji awe amemaliza Kidato cha IV na kupata cheti cha matokeo (School Certificate).
4. Mwombaji awe amepitia mafunzo ya Taaluma yoyote katika ngazi ya kuanzia Astashahada na kuendelea, wenye fani ya Kodi, Biashara au Uhasibu watapewa kipaumbele.
5. Mwombaji awe amehudhuria mafunzo ya kompyuta.



MKURUGENZI HALMASHAURI YA MJI - MAFINGA

CamScanner

6. Awe na wadhamini wawili **(2)** wakazi wa Mafinga wenye mali zisizohamishika.
7. Mwombaji aambatanishe nakala za vyeti vya Elimu na Taaluma kama ilivyoelekezwa hapo juu pamoja na barua za wadhamini zenye namba zao za simu na uthibitisho wa mali zisizohamishika.

**KAZI NA MAJUKUMU**

1. Kukusanya ushuru wa mazao ya, misitu, madini, samaki, minada na ushuru wa vyoo kadri utakavyopangiwa.
2. Kuwasilisha benki fedha iliyokusanywa kila siku.
3. Kuandaa taarifa ya makusanyo na kuiwasilisha Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji – Idara ya Fedha.
4. Na majukumu mengine atakayopangiwa na Mwajiri/Msimamizi wake

**MALIPO/MSHAHARA**

Malipo ya mshahara yatakuwa Tsh. **10,000/=** kwa siku na malipo yatafanyika mwisho wa mwezi.

**2.0: MGAMBO - Nafasi 6**

**SIFA ZA MWOMBAJI**

1. Awe kidato cha IV.
2. Awe amepitia Mafunzo ya Mgambo na kuhitimu, awe na Cheti cha Mafunzo ya Mgambo.
3. Awe raia wa Tanzania.
4. Awe hajawahi kushitakiwa.
5. Awe tayari kufanya kazi yoyote atakazopangiwa na Mwajiri/Msimamizi wake;



MKURUGENZI HALMASHAURI YA

**KAZI NA MAJUKUMU**

1. Kusaidia shughuli za Ukusanyaji wa Mapato na Ulinzi Shirikishi.

**MALIPO/MSHAHARA**

Malipo ya mshahara yatakuwa Tsh. **6,000/=** kwa siku na malipo yatafanyika mwisho wa mwezi, Aidha Mkataba wa kazi hii utadumu kwa muda wa **Miezi Mitatu (3)** tu.

**2. WALINZI – NAFASI 10**

**SIFA ZA MUOMBAJI**

1. Awe kidato cha IV.
2. Awe amepitia Mafunzo ya Mgambo na kuhitimu, awe na Cheti cha Mafunzo ya Mgambo.
3. Awe raia wa Tanzania.
4. Awe hajawahi kushitakiwa.
5. Awe tayari kufanya kazi kituo chochote atakachopangiwa Ndani ya Halmashauri ya Mji.

**KAZI NA MAJUKUMU**

1. Kulinda usalama wa maeneo ya Ofisi.
2. Kulinda usalama wa Rasilimali za Serikali.
3. Kuwasajili wageni wanaoingia Ofisini.

MKURUGENZI HALMASHAURI YA



CamScanner

**MALIPO/MSHAHARA**

Malipo ya mshahara yatakuwa Tsh. **6,000/=** kwa siku na malipo yatafanyika mwisho wa mwezi, Aidha Mkataba wa kazi hii utadumu kwa muda wa **Miezi Mitatu (3)** tu.

## 4.0: WAFANYA USAFI - Nafasi 30

**SIFA ZA MUOMBAJI**

1. Awe raia wa Tanzania.
2. Awe hajawahi kushtakiwa.
3. Awe anajua kusoma na kuandika.
4. Awe na uzoefu wa Utunzaji wa Bustani.
5. Awe na uzoefu wa kufanya kazi ya usafi wa mazingira.

**KAZI NA MAJUKUMU**

1. Kukusanya na kupakia taka kwenye magari ya kusomba taka.
2. Kufanya usafi kwenye maeneo ya Umma.
3. Kupanda na kutunza bustani za maua katika maeneo ya Umma.
4. Kufyeka nyasi ndefu na kusembua katika maeneo ya Umma.
5. Na majukumu mengine utakayopangiwa na Mwajiri/Msimamizi wake.

**MALIPO/MSHAHARA**

Malipo ya mashahara yatakuwa Tsh. **6,000/=** kwa siku na malipo yatafanyika mwisho wa mwezi, Aidha Mkataba wa kazi hii utadumu kwa muda wa **Miezi Mitatu (3)** tu.



MKURUGENZI HALMASHAURI YA

CamScanner

## 5.0: WASAIDIZI UGAVI - Nafasi 2

**SIFA ZA MUOMBAJI**

1. Awe ni Mtanzania na Mkazi wa Mafinga.
2. Awe na umri sio chini ya miaka **18** na sio zaidi ya miaka **45.**
3. Mwombaji awe amemaliza kidato cha IV na kupata cheti cha matokeo (School Certificates).
4. Mwombaji awe na Astashahada/Stashahada ya Manunuzi, Biashara au Uhasibu.
5. Awe na Wadhamini wawili **(2)** wakazi wa Mafinga wenye mali zisizohamishika.

**KAZI NA MAJUKUMU:**

(a) Kutunza ghala la vifaa lenye thamani ndogo.

(b) Kupokea vifaa vipya vitakavyoletwa na wazabuni mbalimbali na kupokea vifaa ambavyo vimetumika lakini vinahitaji kutunzwa kabla ya kufutwa.

(c) Kufungua na kutunza "Bin Card" kwa kila kifaa kilichopo ghalani.

(d) Kufunga "Ledger" ambayo itatunza kumbukumbu ya vifaa vinavoingia kutunzwa na kutoka kwa nyaraka mbalimbali.

(e) Kutoa vifaa kwa wateja na watumiaji wengine.

(f) Kuhakikisha kwamba ghala na vifa vilivyomo vinatunzwa katika hali ya usafi na kwa usalama.

(g) Kufanya kazi zingine atakazopangiwa.

MKURUGENZI HALMASHAURI YA



CamScanner

**MALIPO/MSHAHARA**

Malipo ya mshahara yatakuwa Tsh. **10,000/=** kwa siku na malipo yatafanyika mwisho wa mwezi.

**6.0: MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU II - Nafasi 3**

**SIFA ZA MUOMBAJI**

1. Awe ni raia wa Tanzania.
2. Awe na umri usio chini ya **Miaka 18** na usio zidi **Miaka 45**.
3. Mwombaji awe amemaliza Kidato cha IV na kupata cheti cha matokeo (School Certificates).
4. Awe na cheti cha Utunzaji Kumbukumbu katika fani ya Masijala

**KAZI NA MAJUKUMU**

1. Kuweka kumbukumbu(barua na Nyaraka) katika mafaili.
2. Kupokea na kupeleka majalada sehemu husika
3. Kutafuta kumbukumbu/Nyaraka/mafaili yanayohitajiwa na wasomaji.
4. Kuchambua, kuorodhesha na kupanga kumbukumbu/nyaraka katika makundi kulingana na somo husika (classification and boxing) kwa ajili ya matumizi ya ofisi.
5. Kudhibiti upokeaji, uandikishaji wa kumbukumbu/nyaraka.
6. Na majukumu mengine atakayopangiwa na Mwajiri/Msimamizi.

**MALIPO/MSHAHARA**

Malipo ya mshahara yatakuwa Tsh. **10,000/=** kwa siku na malipo yatafanyika mwisho wa mwezi, Aidha Mkataba wa kazi hii utadumu kwa muda wa Miezi Mitatu (3) tu.



MKURUGENZI HALMASHAURI YA

## 6.0: MPISHI - Nafasi 1

**SIFA ZA MUOMBAJI**

1. Awe ni raia wa Tanzania
2. Awe na umri usio chini ya **Miaka 18** na usio zaidi ya **Miaka 45**.
3. Mwombaji awe amemaliza Kidato cha IV na kupata cheti cha matokeo (School Certificates)
4. Awe na uzoefu wa kazi husika

**KAZI NA MAJUKUMU:**

1. Kupika chakula cha watoto.
2. Kuandaa kuni za kupikia.
3. Kufanya usafi wa vyombo vya kupikia na vyombo na kulia chakula.
4. Kufanya usafi wa eneo la kupikia chakula.
5. Kufanya kazi zingine atakazopangiwa na Mwajiri/Msimamizi wake.

**MALIPO/MSHAHARA**

Malipo ya mshahara yatakuwa **Tsh. 6,000/=** kwa siku na malipo yatafanyika mwisho wa mwezi, Aidha Mkataba wa kazi hii utadumu kwa muda wa **Miezi Mitatu (3)** tu.

## 7.0 MKADIRIAJI MAJENGO (QUANTITY SURVEYOR) – NAFASI 1

**SIFA ZA MUOMBAJI**

1. Awe ni raia wa Tanzania
2. Awe na umri usio chini ya **Miaka 18** na usio zaidi ya **Miaka 45**.
3. Mwombaji awe amemaliza Kidato cha IV AU VI na kupata cheti cha matokeo (School Certificates)



MKURUGENZI HALMASHAURI YA

CamScanner

4. Mwombaji awe na Shahada/Stashahada ya juu ya Uhandisi kutoka katika Vyuo Vikuu vinavyotambuliwa na Serikali katika fani ya Ukadiriaji Majengo.
5. Awe na uzoefu wa kazi husika

**KAZI NA MAJUKUMU:**

(a) Kuratibu miradi ya ujenzi katika ngazi zote (maandalizi, ujenzi na uendeshaji) na kutayarisha program ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi.

(b) Kushirikiana na Wasanifu Majengo katika utekelezaji wa mipango, matokeo ya uvumbuzi na utafiti katika fani zao.

(c) Kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu matumizi kutokana na maendeleo ya teknolojia, na matokeo ya utafiti na uvumbuzi yanayopatikana kwingineko.

(d) Kufanya ukaguzi wa Majengo ikiwa ni pamoja na kuhakiki viwango vya ubora wa Majengo.

(e) Kusimamia utendaji wa kazi wa Wasanifu Majengo walioko chini yake.

**MALIPO/MSHAHARA**

Malipo ya mshahara yatakuwa **Tsh. 15,000/=** kwa siku na malipo yatafanyika mwisho wa mwezi, Aidha Mkataba wa kazi hii utadumu kwa muda wa **Miezi Mitatu (3)** tu.

## 8.0 MHANDISI (CIVIL ENGINEER & ELECTRICAL) –NAFASI 2

**SIFA ZA MUOMBAJI**

1 Awe ni Mtanzania na Mkazi wa Mafinga.

3. Awe na umri sio chini ya miaka **18** na sio zaidi ya miaka **45.**

4. Mwombaji awe amemaliza kidato cha IV au Sita



MKURUGENZI HALMASHAURI YA MJI - MAFINGA

5. Mwombaji awe na Shahada/Stashahada ya juu ya Uhandisi kutoka katika Vyuo Vikuu vinavyotambuliwa na Serikali katika fani ya Ujenzi au Umeme

**KAZI NA MAJUKUMU:**

**MHANDISI UJENZI**

(a) Kufanya ukaguzi wa Barabara, Madaraja na Majengo mbalimbali.

(b) Kuchunguza vyanzo vya ajali barabarani

(d) Kufuatilia utekelezaji wa Sheria na kanuni za ujenzi na matengenezo ya Barabara, Madaraja na Majengo.

(e) Kusimamia na kuratibu kazi za Barabara/Madaraja na Majengo zinazotolewa na Makandarasi

(f) Kutoa ushauri na usimamizi wa kazi za ujenzi wa miradi ya barabara/madaraja na majengo.

(g) Kutayarisha taarifa za maendeleo ya miradi za mwezi, robo, mwaka, nusu mwaka na mwaka mzima ili kueleza maendeleo ya kazi za ujenzi wa Barabara. Madaraja

**MHANDISI UMEME:**

(a) Kuratibu miradi ya Umeme katika ngazi zote (maandalizi, Ujenzi na uendeshaji) na kutayarisha program ya utekelezaji wa- miradi hiyo ya Umeme.

(b) Kufuatilia maendeleo ya teknolojia mbalimbali ya Umeme kwa madhumuni ya kuboresha utaalamu huo kwenye fani hiyo.

(c) Kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu matumizi bora ya umeme kutokana na maendeleo ya teknolojia, na matokeo ya utafiti na uvumbuzi yanayopatikana kwingineko.

(d) Kufanya ukaguzi wa shughuli za Umeme katika majengo ya Halmashauri ikiwa ni pamoja na kuhakiki viwango vya ubora wa huduma zao.



MKURUGENZI HALMASHAURI YA

CamScanner

**MALIPO/MSHAHARA**

Malipo ya mshahara yatakuwa **Tsh. 15,000/=** kwa siku na malipo yatafanyika mwisho wa mwezi, Aidha Mkataba wa kazi hii utadumu kwa muda wa **Miezi Mitatu (3)** tu.

## 9.0 FUNDI SANIFU (UJENZI & UMEME) – NAFASI 3

**SIFA ZA MUOMBAJI**

1. Awe ni raia wa Tanzania
2. Awe na umri usio chini ya **Miaka 18** na usio zaidi ya **Miaka 45**.
3. Mwombaji awe amemaliza Kidato cha IV au VI na kupata cheti cha matokeo (School Certificates)
4. Muombaji awe amefuzu mafunzo ya Ufundi ya miaka miwili kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali katika moja ya fani za ujenzi au umeme au
5. Awe na Stashahada ya kawaida katika fani za ufundi kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali au
6. Awe amehitimu kidato cha IV na kufuzu kozi ya ufundi ya miaka mitatu kutoka Vyo vya ufundi vinavyotambuliwa na Serikali katika mojawapo ya fani za ufundi.

**KAZI NA MAJUKUMU:**

**FUNDISANIFU UJENZI (CIVIL TECHNICIANS)**

(a)Kufanya kazi za ujenzi wa kuta za nyumba na kupaka rangi na kufunga mabomba.

(b)Kuchonga vifaa vya nyumba vya Serikali ikiwa ni pamoja na samani. (Furniture)



MKURUGENZI HALMASHAURI YA

CamScanner

(c) Kufanya kazi za upimaji (survey) wa barabara, majengo na mifereji kama atakavyoelekezwa.

(d) Kufanya kazi za ujenzi wa nyumba za Serikali, barabara na makaravati.

(e) Kusimamia ujenzi wa miradi ya barabara, majengo na madaraja unaofanywa na Wakandarasi.wadogo wadogo.

(f) Kusimamia mafundi wa vikosi vinavyokarabati nyumba za Serikali na barabara.

(g) Kufanya makisio ya gharama na vifaa vya miradi midogo midogo.

(h) Kufanya ukaguzi wa ujenzi wa majengo ya serikali na barabara .

(i) Kuandaa ripoti za utekelezaji wa miradi na kiwango kilichofikiwa kwa kila kipindi cha miezi mitatu mitatu.

(j) Kuandaa makisio ya gharama ya matengenezo ya majengo, barabara na madaraja kwa kila mwaka.

**FUNDISANIFU UMEME:**

(a) Kufanya upimaji wa Umeme kufuatana na maelekezo ya Mhandisi.

(b) Kufanya kazi za kutengeneza vifaa vya umeme.

(c) Kufanga usanifu wa miradi midogo midogo ya Umeme

(d) Kusimamia jinsi ya kufunga mashine mpya zinazotumia Umeme.

(e) Kufanya makisio ya gharama na vifaa kwa miradi midogo midogo ya Kuweka Umeme kwenye nyumba za serikali.

(f) Kufanya matengenezo ya mara kwa mara ya Umeme kwenye nyumba za Serikali.

(g) Kuandaa ripoti za utekelezaji ili kujua kiwango kilichofikiwa, kwa kila kipindi cha miezi mitatu mitatu.

(h) Kuandaa makisio ya gharama ya mahitaji ya vifaa kwa ajili ya vya umeme.



MKURUGENZI HALMASHAURI YA

(i) Kuhakikisha kwamba shughuli za matengnezo ya na vifaa vya umeme inatekelezwa kama ilivyopangwa.

(j) Kutayarisha mpango mzima wa gharama za matengenezo na kushauri uongozi wa juu ipasavyo:-

(k) Kufanya kazi nyingine kama utakavyopangiwa.

**MALIPO/MSHAHARA**

Malipo ya mshahara yatakuwa **Tsh. 15,000/=** kwa siku na malipo yatafanyika mwisho wa mwezi, Aidha Mkataba wa kazi hii utadumu kwa muda wa **Miezi Mitatu (3)** tu.

Maombi yatumwe kwa;

MKURUGENZI WA MJI,
HALMASHAURI YA MJI MAFINGA,
S. L. P. 76,
**MAFINGA**

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **20/06/2022 Saa 9:30 Alasiri**.

Tangazo hili limetolewa na:-

Happiness R. Laizer,
**MKURUGENZI WA MJI,**
**HALMASHAURI YA MJI MAFINGA.**

MKURUGENZI HALMASHAURI YA



MKURUGENZI HALMASHAURI YA